# HOTUBA YA MHE. JOHN ZEFANIA CHILIGATI, (MB.), WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, KWA MWAKA 2010/11

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2010/11.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete** kwa juhudi zake za kusimamia uchumi wa nchi yetu. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais, na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Mpanda Mashariki** kwa kumsaidia

vizuri Mheshimiwa Rais katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kunipatia ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya nne ambapo kwa kushirikiana tumefanikisha miradi mingi ya maendeleo. Vilevile, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge katika Bunge lako Tukufu. Waheshimiwa hao ni Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mhe. Janet Zebedayo Mbene, kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM); na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kutoka Chama cha Wananchi (CUF). Vilevile, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu na Watanzania wote waliopoteza maisha yao kutokana na sababu mbalimbali. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, **Amen.**

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira

chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia (MDGs), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Lengo la msingi la miongozo hiyo ni kuboresha maisha ya wananchi; kudumisha amani, utulivu na umoja; kuimarisha utawala bora; kujenga uchumi madhubuti na endelevu; kuboresha afya; kutunza mazingira na kuboresha makazi. Wizara yangu imetekeleza miongozo hiyo kwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, kutoa hatimiliki za kimila kwa wananchi wa vijijini, na kutoa leseni za makazi kwa wananchi waishio kwenye maeneo yasiyopimwa ili kuwawezesha kukopesheka na kupunguza umaskini.

6. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile Wizara yangu imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa kitaifa pamoja na Bunge.

Maagizo hayo yanayotokana na hotuba za bajeti, maswali na hoja za Waheshimiwa Wabunge; na ahadi mbalimbali za viongozi wa kitaifa.

## MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005 KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2005 – 2010)

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imetekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, hususan ibara ya 42 vifungu (a-d) kuhusu ardhi; ibara ya 68 vifungu (a–h) kuhusu maendeleo ya makazi; na ibara ya 108 kifungu (f) kuhusu sheria ya mabaraza ya ardhi na nyumba. Utekelezaji wa maelekezo ya ibara hizo ni kama ifuatavyo:-

***Ibara ya 42, kifungu (a);***

**Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kwa lengo la kuwawezesha Watanzania kurasimisha ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya benki na mifuko mingine ya fedha inayokopesha.**

8. **Mheshimiwa Spika,** kazi ya kurasimisha ardhi na nyumba nchini iliendelea kutekelezwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Majiji, Miji, Wilaya , MKURABITA na wadau

wengine. Kuanzia Januari 2006 hadi Mei 2010, milki za nyumba **301,961** zilitambuliwa kwenye maeneo yaliyojengwa bila kupimwa mijini. Milki hizo zilitambuliwa katika miji ya Mwanza (nyumba 25,929); Dar es Salaam (265,417), Tanga (3,945), Moshi (1,019) na Dodoma (5,651). Kati ya nyumba zilizotambuliwa, jumla ya leseni za makazi **92,565** zilitolewa. Leseni hizo za makazi zinaweza kutumika kama dhamana kuombea mikopo kwenye taasisi za kifedha.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliongeza kasi ya kupima mashamba na kutoa hatimiliki za kimila *(certificates of customary right of occupancy)*. Kati ya mwaka 2005 na Juni 2010, jumla ya Masjala za Ardhi za Wilaya **25** na Masjala za Ardhi za Vijiji **182** zilikarabatiwa au kujengwa. Hatimiliki za kimila **111,905** zilitayarishwa, kusajiliwa na kutolewa kwa wananchi katika wilaya mbalimbali nchini. Katika kipindi hicho, vyeti vya ardhi ya vijiji **4,227** katika Wilaya **60** za mfano vilisajiliwa na kutolewa, sawa na asilimia 46 ya vijiji vipatavyo 11,000 nchini **(Angalia Jedwali Na. 1).**

*Ibara ya 42, kifungu (b);*

**Kuendeleza kwa nguvu mpya kazi inayofanywa na Halmashauri za Wilaya katika kutambua mipaka ya vijiji na kuvipatia vyeti vya kumiliki ardhi ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote.**

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ilikamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji **5,890** nchini vilivyokuwa havijapimwa. Idadi hiyo imekamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji vyote nchini vipatavyo 11,000. Vilevile, katika kipindi hicho mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji **705** katika wilaya 48 iliandaliwa kupitia mipango shirikishi.

*Ibara ya 42, kifungu (c);*

**Kuendelea kurahisisha taratibu za upatikanaji wa hatimiliki za ardhi.**

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imefupisha muda wa upatikanaji wa hatimiliki, zilikuwa zinachukua zaidi ya mwaka mmoja kutolewa na imefikia lengo la kusajili ndani ya wastani wa siku **180** kama ilivyotamkwa kwenye sheria za ardhi. Hatua zilizochukuliwa kufupisha mchakato huo ni pamoja na kurekebisha taratibu na kuanzisha Ofisi za Ardhi za Kanda sita ambazo ni Mwanza, Dar es salaam, Moshi,

Mbeya, Dodoma na hivi karibuni Mtwara. Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Mei 2010, jumla ya hatimiliki **56,130** zilisajiliwa na kutolewa kwa wananchi **(Angalia Jedwali Na. 2).** Kasi ya utayarishaji na usajili wa hati imeongezeka kutoka hatimiliki **5,464** ilivyokuwa mwaka 2005/06 na kufikia hatimiliki **17,390** mwaka 2009/10.

***Ibara ya 42, kifungu: d (i);***

**Kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu kwa ajili ya kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo.**

12. **Mheshimiwa Spika,** utayarishaji wa ramani za msingi za nchi yetu uliendelea kwa lengo la kuwezesha mipango mbalimbali ya maendeleo kuandaliwa na kutekelezwa. Mipango hiyo ni pamoja na mipango kabambe ya miji, umwagiliaji, utalii, matumizi bora ya ardhi na mazingira. Katika kipindi kilichoanzia Desemba 2005 hadi Mei 2010, ramani za msingi za miji katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Mara, Kigoma, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya na Iringa zilitayarishwa.

***Ibara ya 42, kifungu: d (ii);***

**Kujenga uwezo wa kupata wataalamu na vitendea kazi kwa ajili ya kupima na kutayarisha ramani za maeneo ya maji, maziwa na bahari kupitia Tangazo la Serikali Na. 467 la Desemba 2000.**

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kushirikiana na taasisi za kimataifa za haidrografia ambazo ni *International Hydrographic Organization* (IHO) na *United Kingdom Hydrographic Office* (UKHO) kwa kupatiwa ramani za majini (*hydragraphic charts*) na taarifa zinazohusu usalama majini. Vilevile, ujenzi wa kituo cha kuratibu mawimbi Baharini (*tide gauge*) katika Bahari ya Hindi mjini Mtwara ulikamilika.

***Ibara ya 68, kifungu (c);***

**Kuendelea kuimarisha utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.**

14. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) iliboresha maabara yake kwa kufunga vifaa vipya vya kupima ubora ili kuwezesha upatikanaji wa matokeo bora ya utafiti. Wakala ulizalisha vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na vya gharama nafuu, na ilieneza matokeo ya tafiti zake katika

Wilaya **40.** Vilevile ulitengeneza mashine **450** za kufyatulia matofali ya udongo na saruji yanayofungamana, mashine **110** za kutengenezea vigae vya kuezekea na kalibu (*moulds*) **120** za vigae hivyo. Kazi ya kuhamasisha, kutoa mafunzo, ukandarasi na ushauri wa kitaalam zilifanyika katika halmashauri za wilaya mbalimbali nchini.

***Ibara ya 68, kifungu (d);***

**Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kujenga nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.**

15. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia NHBRA ilitoa mafunzo kwa vitendo na kufanya uhamasishaji kuhusu ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kujenga nyumba za mfano katika Mikoa **19** na Halmashauri za Miji na Wilaya **49.** Kazi hizo zimewawezesha wananchi wengi kuanza kutumia teknolojia bora ya ujenzi inayotumia matofali ya udongo na saruji yanayofungamana. Pia, ushauri wa kitaalam na ukandarasi juu ya utumiaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora vilivyofanyiwa utafiti, ulitolewa katika Wilaya mbalimbali. Wizara iliendelea kushirikiana na makampuni kutoka sekta binafsi kuwezeshwa kuingizwa nchini teknolojia

mpya ya vifaa vya ujenzi wa nyumba vya gharama nafuu. Kwa mfano, kampuni ya Prairies Wind International kutoka Marekani, African Eco Housing ya Uingereza na P&P Developers Ltd ya Dubai walionyesha aina mbalimbali za vifaa vya ujenzi vyenye gharama nafuu.

Aidha, kampuni ya INOVIDA kutoka Ujerumani imejenga Dar es salaam kiwanda cha kutengeneza vifaa vya ujenzi usiotumia saruji, nondo wala mbao kwa lengo la kujenga nyumba za bei nafuu, vifaa hivyo ndivyo vilivyotumiwa kujenga jengo la Wizara la maonyesho ya Nane Nane hapa Dodoma.

***Ibara ya 68, kifungu (f);***

**Kusimamia uanzishwaji wa taasisi za kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba nchini**.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoanzia Desemba 2005 hadi Mei 2010 Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (*Unit Titles Act*) ya mwaka 2008 na Sheria ya Mikopo ya Nyumba ya Mwaka 2008, zilitungwa. Kanuni kwa ajili ya kutekeleza sheria hizo zilikamilika na kuanza kutumika mwezi Mei, 2009. Kazi ya kutoa Elimu kwa umma kuhusu sheria hizo imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari.

Pia, Serikali imeongeza rasilimali kwenye mfuko wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba kwa watumishi wa serikali (*revolving housing loan fund*) ili uweze kuwanufaisha watumishi wengi zaidi.

***Ibara ya 68, kifungu (g);***

**Shirika la Nyumba la Taifa kuendelea kujenga nyumba za makazi na za biashara kwa ajili ya kuuza na kupangisha na kuzifanyia matengenezo zilizo chini yake**.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010 Shirika la Taifa la Nyumba (NHC) liliweka msukumo zaidi katika ujenzi wa nyumba za kuuza kuliko za kupangisha. Uamuzi huu unalenga kuwawezesha wananchi kumiliki nyumba zao wenyewe na hivyo kuzitumia kwa kupata mikopo ya kuendeshea maisha yao. Katika Kipindi husika, jumla ya nyumba na majengo **447** kwa ajili ya kupangisha na kuuza yalijengwa katika miji mbalimbali nchini. Kati ya nyumba na majengo hayo, nyumba **236** ni kwa ajili ya kuuza na majengo makubwa ya vitega uchumi **211** yalijengwa kwa ajili ya kupangisha (**Angalia Jedwali Na. 3a & b**).

18. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010, jumla ya miradi **18** ilitekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Shirika na waendelezaji binafsi. Ujenzi huo unahusisha kuendeleza upya majengo machakavu yaliyopo katikati ya miji mikubwa ili kupendezesha miji kulingana na matumizi bora ya ardhi katika miji yetu. Kutokana na majengo hayo Shirika limejenga nyumba **280** za makazi. Pia, kwenye majengo haya zimejengwa sehemu za ofisi, maduka, vyumba vya hoteli, maghala na viwanda. Kutokana na kutekelezwa kwa miradi ya ujenzi wa majengo hayo, wananchi **1,052** waliajiriwa kwenye nafasi mbalimbali zikiwemo za uhandisi, uchoraji, usimamizi na wafanyakazi katika maduka na viwanda.

19. **Mheshimiwa Spika,** Shirika liliendelea kukusanya kodi ya pango na malimbikizo yake pamoja na kuzifanyia matengenezo nyumba zilizo chini yake. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010, Shirika lilikusanya jumla ya shilingi **bilioni 131.7** kutokana na kodi ya pango la nyumba na malimbikizo yake. Kwa kipindi hiki makusanyo ya kodi na malimbikizo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, mathalan mwaka 2005/06 zilikusanywa jumla ya shilingi **bilioni 19.2** na mwaka 2009/10 zimekusanywa jumla ya shilingi **bilioni 33.**

Kwa upande wa matengenezo, Shirika limekuwa likiyafanyia matengenezo majengo yak**e** **2,332** nchini kote kulingana na mahitaji, umuhimu na uwezo wa Shirika kifedha. Kila mwaka shirika hutenga asilimia 25 ya mapato yake yanayotokana na kodi za pango kwa ajili ya kugharamia matengenezo. Katika kipindi cha Julai 2006 hadi Mei, 2010 jumla ya majengo **2,146** na nyumba (*apartments*) **14,679** zilifanyiwa matengenezo yaliyogharimu shilingi **bilioni 34.8** katika miji mbalimbali nchini**.**

***Ibara ya 68, kifungu (h);***

**Kuendeleza miradi ya kupima viwanja katika miji hasa kwenye Makao Makuu ya Mikoa.**

20. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Halmashauri za miji na wilaya katika kutekeleza miradi ya upimaji wa viwanja mijini. Katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Mei, 2010, Halmashauri za miji **48** zilikopeshwa jumla ya shilingi **bilioni 6.9** kupitia mfuko wa mzunguko wa kupima viwanja (*Plot Development Revolving Fund* (PDRF)) ambapo hadi Juni, 2010 jumla ya viwanja **25,094** vilipimwa. Hadi Juni 2010 Halmashauri 21 kati ya 42 zimerejesha jumla ya Shilingi **306,428,932.80** ikiwa ni pamoja na riba ya asilimia ishirini. Aidha, kupitia mradi wa Kupima

Viwanja 20,000, jumla ya shilingi **bilioni 3.3** zilikopeshwa kwenye halmashauri kwa ajili ya kupima viwanja na kuwagawia wananchi. Katika kipindi kilichoanzia Julai 2006 hadi Mei 2010, Jumla ya viwanja **59,614** vimepimwa katika miji ifuatayo: Jiji la Dar es Salaam (41,000); Mwanza (10,000), Morogoro (2,764), Mbeya (2,350), Kibaha (500) na Bagamoyo (3,000).

***Ibara ya 108, kifungu (h);***

**Kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hususan Ujenzi wa Majengo ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Ngazi za Wilaya na kuajiri Mahakimu wa kutosha**.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi kilichoanzia Julai, 2006 hadi Aprili 2010, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 16 yaliundwa na Wenyeviti 29 waliajiriwa. Katika kipindi hicho jumla ya mashauri **40,287** yalifunguliwa na mashauri **26,865** yalisikilizwa na kuamuliwa.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2009/10 NA MALENGO YA MWAKA 2010/11

### Ukusanyaji wa Mapato

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ina jukumu la kukusanya ada mbalimbali zinazotozwa kupitia umiliki wa ardhi. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya **shilingi 15,550,006,000** kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2010, jumla ya **shilingi 11,642,119,118.98** ambazo ni sawa na **asilimia 75** ya lengo zimekusanywa. Kati ya makusanyo hayo, **shilingi 10,430,902,549** ambazo ni sawa na **asilimia 90** ya makusanyo ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja na mashamba. Upungufu wa makusanyo ya maduhuli umetokana na udhaifu uliopo katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2010/11, Wizara ina lengo la kukusanya kiasi cha **shilingi 20,641,200,000.** Maduhuli haya yatakusanywa kwa kutumia mikakati ifuatayo:- kukijengea uwezo kitengo cha ukusanyaji wa maduhuli; kuhakikisha kila mmiliki wa kiwanja analipa kodi stahili kulingana na matumizi yake; kuboresha kumbukumbu za ardhi;

kuongeza wigo wa walipa kodi ya ardhi kwa kupima viwanja na kukamilisha upimaji katika maeneo mbalimbali, kuelimisha wananchi juu ya wajibu wao wa kulipa kodi ya ardhi kila mwaka; kurahisisha utaratibu wa malipo; kujenga kituo cha huduma kwa wateja; kuhakikisha huduma zinapatikana pale zinapohitajika ikiwa ni pamoja na ramani kwa ajili ya matumizi mbalimbali na, kufuatilia kwa karibu vituo vya makusanyo ili kudhibiti mapato kwa mujibu wa sheria za fedha. **Ninatoa wito kwa wamiliki wa ardhi nchini kulipa kodi za pango la ardhi na ada zingine** kwa wakati.

**Matumizi**

24. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi **33,483,299,000.** Kati ya fedha hizo shilingi **5,962,158,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi **15,507,598,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi **12,013,543,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Juni 2010 jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi **26,261,423,816.** Kati ya fedha hizo, shilingi **11,952,752,127** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi **5,950,436,058** ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **8,358,235,631** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Juni 2010, kiasi kilichotumika ni shilingi **25,963,529,778**.

## MAENDELEO YA ARDHI

25. **Mheshimiwa Spika**, ardhi ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi wa nchi na ni muhimili wa shughuli mbalimbali mijini na vijijini. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Wizara yangu inaendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi kwa lengo la kuimarisha uhakika na usalama wa milki. Huduma hizo ni pamoja na kutoa hatimiliki za ardhi, kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma, na kutatua migogoro ya ardhi kiutawala.
Aidha, Wizara inashughulikia uhamasishaji wa uanzishaji wa masjala za ardhi za wilaya na vijiji kwa lengo la kusajili na kuhifadhi vyeti vya ardhi ya kijiji, hatimiliki za kimila, pamoja na kutoa elimu ya sheria za ardhi kwa wananchi.

**Utoaji Milki**

26. **Mheshimiwa Spika**, mchakato wa kuandaa hatimiliki za ardhi unaanzia kwenye ngazi za Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya na kwa sasa unaishia katika ofisi za Kanda. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ililenga kutoa hatimiliki **20,000** ambapo lengo hili lilivukwa kwa kutoa hatimiliki **22,491**. Ningependa kuzipongeza Halmashauri ambazo zimeonyesha juhudi kubwa za kuandaa hatimiliki katika mwaka wa fedha 2009/10. Halmashauri hizo ni: - Jiji la Mwanza, Manispaa za Kinondoni, Ilala, Arusha na Arumeru. Pongezi hizi pia

ziwaendee, Waheshimiwa wabunge, viongozi wa mikoa na wilaya kwa kuhimiza kazi hiyo.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10 Wizara yangu iliahidi kufungua ofisi ya ardhi Kanda ya Kusini Mashariki, mjini Mtwara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa ofisi ya ardhi ya kanda ya Kusini Mashariki mjini Mtwara tayari imefunguliwa na imepatiwa watumishi na vitendea kazi, na imeanza kutoa huduma, hivyo kufikisha kanda sita. Kwa mwaka wa fedha 2010/11 Wizara yangu itafungua ofisi ya ardhi ya kanda ya magharibi mjini Tabora itakayohudumia mikoa ya Tabora, Shinyanga na Kigoma. **Ninatoa wito kwa wananchi, viongozi na watendaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri waendelee kutoa ushirikiano na kuhakikisha kuwa ofisi hizo zinatoa huduma kwa wananchi bila usumbufu na ucheleweshaji kama ilivyokusudiwa.**

**Ukaguzi na Uhakiki wa Milki**

28. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Wizara yangu iliendelea na utatuzi wa migogoro ya ardhi na kushughulikia kero mbalimbali za wananchi kuhusu ardhi. Migogoro ya aina hiyo ilitatuliwa kwa njia za kiutawala na iliposhindikana wahusika walishauriwa kwenda kutafuta haki zao mahakamani.

Migogoro hiyo inatokana na wananchi kughushi nyaraka za umiliki, ugawaji wa kiwanja kwa zaidi ya mtu mmoja, wamiliki wa asili kutokulipwa fidia, na wananchi wenye milki halali kuacha kuendeleza viwanja walivyomilikishwa kwa wakati. Wizara imeimarisha matumizi ya tecknolojia ya kompyuta katika uandaaji wa hati na utunzaji wa kumbukumbu za miliki ya viwanja ili kupunguza migogoro hii.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, jumla ya milki **4,500** zilihakikiwa na kukaguliwa katika maeneo ya Mbezi, Jangwani Beach, Tegeta, Ununio na Boko Jijini Dar es Salaam. Kutokana na uhakiki huo nyaraka mpya za umiliki kwa viwanja **4,098** kati ya 5,000 vilivyokusudiwa zilitolewa. Zoezi la uhakiki katika maeneo haya limehusisha kuweka miundombinu ya barabara zenye urefu wa kilometa 50.8. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, wizara yangu itakamilisha uhakiki na ukaguzi wa milki za viwanja **4,018** zilizobakia. Napenda kutoa tahadhari kwa wananchi wanaonunua ardhi katika maeneo hayo wahakikishe kuwa milki hizo zimehakikiwa na Wizara kabla ya kufanya maamuzi ya malipo ili kuepuka hasara inayoweza kupatikana kutokana na udanganyifu. Aidha, **nawaarifu wamiliki wote wa viwanja katika maeneo hayo ambao hawajawasilisha nyaraka za umiliki wa ardhi, wawasilishe**

**Wizarani nyaraka hizo kwa ajili ya uhakiki na kupatiwa nyaraka mpya kwa vile zoezi hili litakamilika mwaka wa fedha 2010.**

**Utwaaji na Ubatilishaji Milki**

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi na sheria za ardhi kila mwananchi anayemilikishwa ardhi anawajibu wa kulinda mipaka ya ardhi yake, kuiendeleza na kulipa kodi ya pango la ardhi. Mwananchi anayeshindwa kutekeleza masharti hayo serikali ina haki ya kubatilisha umiliki wake kwa mujibu wa sheria za nchi. Aidha, ardhi inapohitajika kwa manufaa ya umma hutwaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Utwaaji wa Ardhi Na. 7, 1967 (Sura Na. 118). Katika mwaka wa fedha 2009/10 milki za wananchi 52 zilitwaliwa na kubatilishwa. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kushughulikia utwaaji na ubatilisho wa milki za wananchi wanaoshindwa kutekeleza masharti ya uendelezaji.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10 Wizara ilitoa vibali vya uhamisho wa milki **351** na rehani **98** kati ya lengo la kutoa vibali vya kuweka rehani na uhamisho kwa miliki **400** katika jiji la Dar es Salaam. Vilevile kazi hizo ziliendelea kutekelezwa kwenye halmashauri nchini. Kwa

mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inakusudia kushughulikia na kutoa vibali vya kuweka rehani na uhamisho kwa milki **1,000**.

**Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji**

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5, 1999 (Sura 114), katika Wilaya zilizochaguliwa kutekeleza miradi ya mfano, wilaya hizo ni Babati, Bariadi, Namtumbo na Manyoni. Utekelezaji wa miradi hiyo una lengo la kuhakikisha mipaka ya vijiji imepimwa na kupatiwa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji *(Certificates of Village Land),* kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, kupima na kumilikisha mashamba ya wananchi kwa kuwapatia Hati za Hakimiliki ya Kimila *(Certificates of Customary Right of Occupancy).*

33. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10 Wizara iliahidi kujenga masjala za ardhi za vijiji 92 na masijala za ardhi za Wilaya 15 na kusajili hatimiliki za kimila 100,000. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Juni, 2010 jumla ya masjala za wilaya 15 na za vijiji 61 zilijengwa au kukarabatiwa kwa kushirikiana na Halmashauri, Ofisi ya Rais (MKURABITA) na wadau mbalimbali wa ardhi. Jumla ya vyeti vya ardhi ya vijiji **3,296** na hatimiliki **93,400** zilisajiliwa na

kutolewa kwa wananchi katika wilaya za Babati, Bariadi, Namtumbo na Manyoni **(Angalia Jedwali Na. 4)**. Kwa mwaka wa fedha 2010/11 Wizara itasimamia uandaaji na usajili wa vyeti vya ardhi ya vijiji **5,000;** hatimiliki za kimila zipatazo **138,000** katika vijiji 138 vilivyosalia kwenye Wilaya za mfano za Babati na Bariadi na vijiji vingine nchini.

**Elimu kwa Umma**

34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau mbalimbali iliendelea kutoa elimu ya sera na sheria zinazohusu majukumu ya sekta ya ardhi. Elimu hiyo ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambavyo ni redio, televisheni, pia kupitia ushiriki katika maonesho ya wiki ya utumishi wa umma na nane nane. Aidha, Wizara ilikamilisha utayarishaji wa mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuchapisha **nakala 5,000.** Mwongozo huo utatumika kutoa elimu kwa umma katika ngazi za vijiji wakati wa maandalizi ya kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itachapisha nakala za mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kutoa elimu kwa umma kuhusu

sera na sheria zinazosimamia sekta ya ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya.

**Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria:**

35. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilijiwekea lengo la kusajili hati za kumiliki ardhi pamoja na nyaraka za kisheria zipatazo **42,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa lengo hilo limevukwa kwa kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria **45,559**. Kati ya hizo hatimiliki **17,390** pamoja na nyaraka **18,974** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334 (**Angalia Jedwali Na. 5a**); Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria Sura Na. 117 ni **8,275,** Sura Na.210 ni **920** (**Angalia Jedwali Na. 5b**). Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara ina lengo la kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria **50,000**. Kati ya hizo **20,000** ni hatimiliki na **30,000** ni nyaraka za kisheria.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikuwa na lengo la kufanyia marekebisho ya sheria za Usajili wa Hati (Sura ya 334) na Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) ili kuboresha shughuli za usajili. Mtaalam mwelekezi aliyeteuliwa kufanya utafiti na kutoa mapendekezo ya namna ya kuimarisha mchakato wa usajili wa hati na

utunzaji wa kumbukumbu pamoja na marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334) amekwishawasilisha mapendekezo yake. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara yangu itaanzisha mfumo wa usajili wa elektroniki (*Land Registration System*) utakaoboresha uwekaji kumbukumbu na kuifanyia marekebisho sheria ya usajili wa ardhi (Sura 334) ili iendane na wakati. Vilevile, wizara itaanzisha Ofisi ya Msajili wa Hati Kanda ya Tabora ili kupeleka huduma karibu na wananchi ambao hivi sasa wanapata huduma katika ofisi iliyopo Mwanza. Kanda hiyo mpya itahudumia mikoa ya Tabora, Kigoma na Shinyanga.

**Uthamini wa Mali**

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliendelea na kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuthamini nyumba na mali nyinginezo kwa ajili ya kulipa fidia, kutoza kodi ya ardhi, mauzo (*transfer*), mizania (*balance sheet*) kuomba mikopo, mirathi na bima. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ililenga kufanya uthamini na kuidhinisha taarifa za uthamini wa nyumba na mali nyinginezo 10,000. Hadi Juni 2010 jumla ya nyumba na mali nyingine **7,386** zilithaminiwa na kuidhinishwa. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inakusudia kufanya uthamini na kuidhinisha taarifa zipatazo

12,000. Vilevile, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/10 niliahidi kutayarisha rasimu ya sheria ya kusimamia kazi za uthamini (*Valuation Bill*) na Sheria ya Wakala wa Milki (*Real Estate Agency*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Miswada hiyo imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano ujao wa Bunge.

**Viwango vya Fidia**

38. **Mheshimiwa Spika,** viwango vya fidia hupatikana kwa kuzingatia mahali ardhi ilipo, maendelezo na gharama zingine na uthamini wake hufanyika kulingana na matakwa ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Hata hivyo, Wizara imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wanaolazimika kuachia maeneo yao kwa ajili ya kuruhusu uendelezaji wa maeneo hayo kwa shughuli mbalimbali za kiserikali na hata uwekezaji binafsi. Malalamiko hayo ni kuhusu kiwango duni cha fidia kinachotolewa. Katika mwaka wa fedha 2009/10, wizara imefanya utafiti wa gharama za fidia za mazao na ardhi katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kufanya tafiti katika mikoa iliyobaki ili kuwa na mwongozo wa viwango vya fidia unaozingatia gharama halisi za soko kwa lengo la kuboresha viwango vya fidia na kumaliza malalamiko ya wananchi kuhusu suala la fidia.

**Kuanzishwa kwa Hazina ya Ardhi (*Land Bank*)**

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kuratibu uanzishwaji wa Hazina ya Ardhi *(Land Bank)* kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa Hazina ya Ardhi ni sehemu muhimu ya kuwezesha uwekaji wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii, maendeleo ya Miji na utekelezaji wa kaulimbiu ya kitaifa ya **"Kilimo Kwanza".** Katika mwaka 2009/10 uhakiki na ukaguzi wa mashamba 72 yaliyotelekezwa na wawekezaji ulifanyika katika Mkoa wa Morogoro wa mashamba matano. Taratibu za kufuta milki za mashamba hayo zinaendelea ili yaweze kugawiwa kwa wawekezaji wa ndani na nje ili yatumike kwa shughuli za maendeleo.

40. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya itafanya uhakiki wa mashamba yote nchini yaliyotelekezwa na kuyaandalia mipango mipya ya uendelezaji. Kwa upande wa viwanja mijini, Wizara itashirikiana na Halmashauri zenye mahitaji makubwa ya uwekezaji kupima viwanja kwa ajili hiyo. Ninaendelea kusisitiza kuwa ardhi itakayoingizwa kwenye Hazina ya Ardhi itakuwa imeandaliwa mipango ya matumizi ya

ardhi yenye kuzingatia maslahi ya wanavijiji na sharti ipimwe. Hivyo, ardhi hiyo haitahusisha mashamba ya wanavijiji na haitaathiri mahitaji ya baadaye ya ardhi kwa wanavijiji. **Natoa wito kwa Halmashauri za miji na Wilaya nchini kuendelea na uhakiki wa mashamba yaliyotelekezwa kwa kutuma ilani kwa wamiliki wake na kuwasilisha mapendekezo ya ufutaji wa milki. Kwa upande wa mijini, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za miji itaendelea kupima viwanja kwa ajili ya matumizi mbalimbali kulingana na mahitaji ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.**

## KUMBUKUMBU ZA ARDHI NA MAWASILIANO

41. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Wizara iliendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha kumbukumbu za ardhi kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi, mifumo ya habari na mawasiliano. Wizara iliendelea kuhifadhi kumbukumbu za viwanja na mashamba kwa kutumia mfumo wa kompyuta wa *Management of Land Information System* (MOLIS) na kukadiria kodi za ardhi kwa kutumia mfumo wa *Land Rent Management System* (LRMS). Katika mwaka wa fedha 2009/10, ofisi za ardhi katika Halmashauri nane za Kilombero, Bunda, Arusha, Mufindi, Geita, Moshi, Nzega na Bagamoyo zilipatiwa mafunzo ya kutumia mfumo wa kukadiria kodi na

kuimarisha kumbukumbu kwa kutumia kompyuta. Kutokana na juhudi hizo, hadi kufikia Mei 2010, jumla ya kumbukumbu za wamiliki 32,301 zilihifadhiwa katika kompyuta. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara yangu ina mkakati wa kuziwezesha Halmashauri zingine nane kuweka mfumo wa kompyuta wa kukadiria kodi.

42. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2009/10, tafiti mbili zenye lengo la kuboresha huduma kwenye sekta ya Ardhi zilifanyika, tafiti hizo zilihusu utoaji wa huduma katika ofisi ya Msajili wa Hati (*needs assessment for the registry of titles)* iliyofanywa na kampuni ya SwedSurvey ya Sweden kwa kushirikiana na International Land System (ILS) ya Marekani; huduma katika ofisi ya Kamishna wa Ardhi (*systems reform in the office of the Commissioner for Lands)* iliyofanywa na kampuni ya kizalendo ya InfoBridge Consultants Limited. Madhumuni ya tafiti hizi ni kuwa na mfumo mmoja wa kumbukumbu za ardhi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2010/11 mapendekezo ya tafiti hizi mbili yatafanyiwa kazi kwa lengo la kuwa na mfumo mmoja utakaorahisisha utoaji wa huduma katika sekta ya Ardhi (*integrated database system*).

## MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

43. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara iliendelea kuboresha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya **39** yaliyoanzishwa kwa kuyapatia watumishi na magari mabaraza 21 yaliyopo katika makao makuu ya mikoa. Katika kipindi hicho, watumishi **38** wa kada mbali mbali waliajiriwa. Aidha, ofisi za Mabaraza **9** za Wilaya ya Temeke, Ilala, Kinondoni, Songea, Morogoro, Kigoma, Musoma, Mtwara na Mwanza zilifanyiwa ukarabati. Vilevile katika kipindi hicho, jumla ya mashauri **9,219** yalifunguliwa, kati ya hayo mashauri **7,756** yaliamuliwa na **12,735** yanaendelea kushughulikiwa **(Angalia Jedwali Na. 6).** Katika mwaka wa fedha 2010/11 Wizara itaanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika Wilaya za Nzega, Kilosa, Manyoni na Ngorongoro. Uanzishaji wa mabaraza haya unakwenda kwa kasi ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Mabaraza yenye mashauri mengi yataongezewa idadi ya vikao kutoka viwili hadi vitatu kwa wiki kwa lengo la kupunguza mlundikano wa kesi. Aidha, posho ya Wazee wa Baraza itaongezwa kutoka shilingi 20,000 kwa siku za kikao za sasa hadi shilingi 30,000 kwa kikao kwa siku.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilipitia upya mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na

nyumba, na kuchunguza chanzo cha migogoro kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi katika Mabaraza katika ngazi ya Wilaya. Wizara pia iliendelea kutoa Elimu kwa umma juu ya Sheria Namba 2 ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ya Mwaka 2002 *(The Land Disputes Courts Act, 2002)* kupitia vyombo vya habari, katika maonesho ya wakulima na wiki ya Utumishi wa umma. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Halmashauri za wilaya itaendelea kutoa elimu juu ya Sheria Namba 2 ya mwaka 2002 katika ngazi za Wilaya, Kata hadi Vijijini. Elimu itakayotolewa itawajengea uwezo wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ili waweze kutoa haki kwa wananchi katika migogoro wanayoshughulikia. Uelewa wa sheria hii utawapunguzia wananchi usumbufu katika kutafuta haki zao na hivyo kuelekeza nguvu zao katika shuguli za uzalishaji mali.

## HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

45. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa majukumu ya kusimamia upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi nchini. Upimaji ardhi huwezesha kupata vipimo, ukubwa na mipaka ya vipande vya ardhi, taarifa na takwimu ambazo ni msingi wa usimamizi wa ardhi katika sekta zote.

**Utayarishaji wa Ramani**

46. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/10 wizara iliahidi kukamilisha uhakiki na utayarishaji wa ramani za vitalu vya Kagera; Kigoma; Musoma na Mbeya na miji 10 ya kanda ya magaharibi. Kazi hiyo ilikamilika katika vitalu vya Kigoma, Musoma, Songea na Mbeya. Kazi ya utayarishaji wa ramani katika kitalu cha Kagera inaendelea. Kazi zingine zilizotekelezwa ni upimaji picha (*ground photo control*) na uhakiki ardhini kwa ajili ya utayarishaji wa ramani za msingi katika miji 15 ya kanda ya kaskazini mashariki inayohusisha mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani , Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Dodoma**.** Aidha, uhakiki ardhini katika vitalu vya Kigoma na Ruvuma ulikamilika na utayarishaji wa ramani ya Wilaya ya Nzega katika uwiano wa 1:350,000 unaendelea. Kwa mwaka 2010/11, Wizara itatumia picha za anga (*satellite imagery*) kwa ajili ya kuhuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:2,500 katika miji kumi (10) ya kanda ya magharibi inayohusisha Mikoa ya Mbeya, Tabora, Rukwa na Kigoma. Pia, uchapaji wa ramani utaboreshwa kwa kufunga mtambo mpya wa kisasa wenyekutoa ramani zenye ubora.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaanza kujenga kituo cha kupokelea picha za Satilaiti

(*Direct Satellite Receiving Station*) mjini Dodoma. Kujengwa kwa kituo hiki kutarahisisha upatikanaji wa takwimu za ardhi na ramani mbalimbali ambazo zitatumika kutayarisha mipango ya maendeleo ikiwemo ya upimaji wa mashamba ya wananchi. Picha za *satellite* zitatumika pia na vyombo vya ulinzi na usalama, utabiri wa hali ya hewa, na utengaji wa maeneo katika zoezi lijalo la sensa ya watu. Aidha, Serikali itaongeza mapato yatokanayo na kuuzwa kwa picha za *satellite* katika nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini.

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea na mchakato wa kujenga alama za mtandao mpya wa alama za msingi za upimaji ardhi (*National Geodetic Control Network*). Mtandao huu utapunguza gharama za upimaji wa ardhi na kuwawezesha wananchi wengi kupimiwa mashamba yao. Katika mwaka 2009/10, Wizara iliahidi kusimika alama 300 za msingi za upimaji ardhi ambapo hadi kufikia Juni, 2010 jumla ya alama za msingi **387** zimesimikwa nchini. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itasimika na kupima alama **nyingine 300** katika wilaya mbalimbali nchini hususan Kanda ya Kusini na Kusini Magharibi mwa nchi yetu.

**Sera ya Upimaji na Ramani**

49. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2008/09 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ilikuwa imeanza kuaandaa Sera ya Taifa ya Upimaji na Ramani na ilitarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2009/10. Hadi Juni, 2010 rasimu ya sera hiyo iliwasilishwa kwa wadau na hivi sasa inaendelea kufanyiwa maboresho kwa kuzingatia michango iliyotolewa na wadau. Matarajio ya Wizara ni kuhakikisha kuwa sera hiyo inakamilishwa mwaka wa fedha 2010/11.

**Mipaka ya Ndani ya Nchi**

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inalo jukumu la kutafsiri mipaka ya Vijiji, Wilaya na Mikoa kwa mujibu wa matangazo husika ya serikali (*Government Notices*). Uzoefu unaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya mipaka hiyo ni wananchi katika baadhi na vijiji na wilaya kutotambua mipaka iliyowekwa rasmi na kutafsiriwa kwenye matangazo ya serikali (GN). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri, Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliweza kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala kati ya Halmashauri ya Geita na Hifadhi ya Msitu wa Geita; Kijiji cha Shume Magamba na Hifadhi ya

Msitu wa Shume Magamba; kati ya vijiji na Hifadhi za Taifa za Mikumi, Selous na Serengeti, pia, kati ya wilaya ya Sikonge na Manyoni kwa kutafsiri GN za mipaka hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kushirikiana na TAMISEMI na Maliasili na Utalii kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa.

**Mipaka ya Kimataifa**

51. **Mheshimiwa Spika,** uimarishaji wa mipaka ya kimataifa unafanywa kwa ushirikiano kati ya nchi zinazopakana. Katika mwaka 2009/10, Wizara ilipanga kuhakiki na kuongeza alama za mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imeanza kutekelezwa katika eneo la nchi kavu katika Ziwa Nyasa kwenye makutano ya Mito Misinje na Ruvuma kwa kukagua alama za mipaka zilizoharibika na kuzijenga upya na kuongeza alama zingine za mpaka mahali ambapo alama hizo ziko mbali. Vilevile, mikutano ya kujadili mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani za Msumbiji, Shelisheli, Comoro na Kenya ilifanyika. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, kazi ya kuhakiki, kukarabati na kuongeza alama zingine za mpaka kati ya Tanzania na Msumbuiji; na Tanzania na Kenya itatekelezwa. Aidha, mazungumzo ya

mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa yatafanyika.

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

52. **Mheshimiwa Spika,** Maendeleo nchini yataletwa baada ya kila kipande cha ardhi kutambuliwa, kupimwa mipaka yake na kumilikishwa kwa mmiliki mmoja mmoja au vikundi. Umilikishaji huo unategemea kutambuliwa kwa mipaka kati ya kijiji na kijiji. Katika mwaka 2009/10, Wizara yangu iliahidi kupima mipaka ya vijiji 1,500 vilivyokuwa havijapimwa nchini. Hadi Juni, 2010 vijiji vyote **1,604** vilikuwa vimepimwa katika mikoa ya Kilimanjaro (93), Singida (316), Mara (351), Mwanza (33), Kagera (284), Kigoma (21), Tabora (127), Shinyanga (243), Dodoma (54), Manyara (5) na Morogoro (87) **(Angalia Jedwali Na. 7**). Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji vipya 300 vilivyoongezeka mwaka 2009.

**Upimaji wa Ardhi Chini ya Maji**

53. **Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Wizara ni upimaji wa ardhi chini ya maji na kutayarisha ramani zinazoonyesha umbile la ardhi iliyo chini ya maji hususan milima, mabonde, miinuko na kina cha maji. Ramani hizi

hutumika kuongozea vyombo vya majini na matumizi mengine. Katika mwaka 2009/10, Wizara ilijenga kituo cha kuratibu mawimbi Baharini *(tide gauge)* kando kando ya Bahari ya Hindi eneo la Mtwara. Kujengwa kwa kituo hiki kutasaidia kuratibu na kutoa taarifa mbalimbali muhimu zinazohusu hali ya Bahari *(early warning system).* Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya hydrografia itaendelea kujenga uwezo wa kupima ndani ya maji kwa kuwasomesha wataalam na kuimarisha kituo cha kuratibu mawimbi Baharini cha Mtwara.

**Kuongeza Ukanda wa Kiuchumi Baharini**

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ilikamilisha andiko la awali la kuongeza ukanda wa kiuchumi Baharini (*Exclusive Economic Zone*) na kuliwasilisha Umoja wa Mataifa tarehe 13 Mei, 2009. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itakamilisha andiko la kuongeza ukanda wa kiuchumi Baharini na kuliwasilisha rasmi kwenye Umoja wa Mataifa. Tanzania ilipewa tarehe ya mwisho kuwasilisha andiko kamili kuwa 13 Mei, 2011.

**Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

55. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/10, Wizara iliidhinisha upimaji wa viwanja **37,820** na mashamba **609** kati ya lengo la viwanja vipatavyo 35,000 na mashamba 1,000 kwa mwaka **(Angalia Jedwali Na. 8).** Aidha, katika juhudi za kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, jumla ya ramani za viwanja 15,116 zimepigwa picha (*scanned*) na kuhifadhiwa kwenye mfumo wa elektroniki. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inatarajia kuidhinisha upimaji wa viwanja 50,000 na mashamba 100 kutoka Halmashauri mbalimbali nchini na kuendeleza kazi ya kupiga picha (*scanning*) ramani za viwanja na mashamba.

56. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2009/10, Wizara ingekasimu madaraka ya kusimamia na kuidhinisha upimaji viwanja na mashamba katika ngazi za kanda. Wizara imekamilisha tathmini ya mahitaji na maandalizi ya kukasimu mamlaka ya kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba katika ngazi za kanda. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itakasimu mamlaka ya kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba katika kanda sita (6) za sekta ya ardhi ambazo ni Kanda ya Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kaskazini (Moshi), Ziwa (Mwanza), Kusini

Mashariki (Mtwara) na Magharibi (Tabora). Ili kufanikisha azma hiyo, wataalam wa upimaji na ramani wenye sifa zinazotambulika na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi (*National Council of Professional Surveyors*) watahitajika sana kwa ajili ya kukagua kazi zote za upimaji ardhi kabla ya kuziwasilisha kwenye ofisi za kanda kwa ajili ya kuidhinishwa.

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu itatoa kipaumbele katika kuboresha kumbukumbu za ardhi zikiwemo za upimaji wa ardhi ambazo zinaongezeka kila siku kutokana na uzalishaji wa viwanja vipya. Ili kukabiliana na changamoto hiyo Wizara imepanga kuanzisha mfumo mpya wa kielekitroniki wa utunzaji kumbukumbu za upimaji ardhi (*Cadastral Survey Information System*) utakaowezesha upatikanaji wa taarifa za ardhi kwa urahisi na kuboresha utoaji wa huduma za upimaji ardhi nchini. Mfumo huu utaunganisha shughuli zote za utoaji huduma za ardhi makao makuu, ofisi za kanda, mikoa na halmashauri za miji na wilaya.

**MIPANGO YA MIJI NA VIJIJI**

58. **Mheshimiwa Spika**, upangaji na usimamiaji wa uendelezaji wa miji na vijiji hapa nchini hufanyika kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na ya

Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na Sheria zinazohusika na uendelezaji wa miji. Sheria hizo ni pamoja na sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, Sheria ya kusimamia taaluma za maafisa mipangomiji Na. 7 ya mwaka 2007 na Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 pamoja na miongozo yake.

**Uandaaji na Utekelezaji wa Mipango ya Uendelezaji Miji**

59. **Mheshimiwa Spika**, idadi ya watu wanaoishi mijini nchini imeongezeka kutoka 786,567 (sawa na asilimia 6) mwaka 1967, hadi 7,943,561 (sawa na asilimia 23.1) mwaka 2002 na inakadiriwa kufikia watu 12,000,000 (sawa na asilimia 30) mwaka 2010. Idadi hiyo inatarajiwa kufikia zaidi ya watu 30, 000,000 (sawa na asilimia 50) ifikapo mwaka 2025. Kasi hiyo, kubwa ya ongezeko la watu mijini ni changamoto kwa mamlaka za upangaji miji kukidhi mahitaji ya msingi kwa watu hao.

60. **Mheshimiwa Spika,** Katika upangaji wa miji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na miji huandaa mipango ya jumla (*General Planning Schemes*) ya aina mbili ya kuongoza uendelezaji wake. Mipango hiyo ni ile ya muda mrefu (*master plans*) ambayo hutoa mwongozo wa uendelezaji kwa miaka ishirini na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda mfupi

ambayo ni ya miaka kumi. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Mbarali, Manyoni, Kahama na Isaka ilikamilisha mipango ya muda mfupi. Aidha, mipango kabambe ya Jiji la Tanga na Mji wa Bagamoyo inaendelea kuandaliwa. Kwa mwaka 2010/11, wizara itaandaa mipango ya muda mfupi ya miji ya Misenyi, Geita na kuhuisha mpango wa Makambako. Vilevile, uhuishaji wa mpango kabambe wa Jiji la Dar es Salaam utafanyika.

61. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali pia huandaa mipango ya uendelezaji upya maeneo mbali mbali ya miji (*Redevelopment Schemes)*. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Mpango wa uendelezaji upya eneo la kati la Manispaa ya Temeke ulikamilika. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Songea itakamilisha mpango wa uendelezaji upya eneo la kati na kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni itaandaa mpango wa uendelezaji upya eneo la Kinondoni.

62. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kupanua ukubwa wa eneo la Bandari ya Dar es Salaam, ili liweze kuhudumia mizigo mingi zaidi, eneo la Kurasini lilipangwa na kutengwa ili liweze kutoa huduma zinazoendana na shughuli za bandari.

Katika mwaka 2009/10, Wizara ilithamini na kuhakiki mali **191** na kulipa fidia ya kiasi cha shilingi **bilioni 6** kwa wananchi wa Mtaa wa Mivinjeni ili kupisha upanuzi wa bandari, wananchi hawa walipewa viwanja mbadala eneo la Kibada. Kutokana na ulipaji wa fidia hiyo eneo huru lenye ukubwa wa ekari 8.7 lilipatikana na kupimwa viwanja vikubwa kwa ajili ya matumizi yanayoendana na shughuli za bandari. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, kazi ya ulipaji wa fidia, upimaji wa viwanja na umilikishaji wa eneo lenye jumla ya ekari 21 utatekelezwa.

**Urasimishaji**

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura Na. 113 na Sheria ya Mipangomiji Na. 8, 2007 zinaelekeza kurasimisha maeneo yaliyojengwa bila kupimwa kwa kushirikiana na halmashauri za miji na wilaya. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilishirikiana na Jiji la Mwanza kutambua miliki **19,876** katika maeneo yaliyojengwa bila kupimwa na kuandaliwa mipango ya urasimishaji. Kupitia mradi wa urasimishaji unaotekelezwa Jijini Mwanza jumla ya viwanja takribani **7,000** vimepimwa na hati **518** kuandaliwa na wananchi **135** walimilikishwa kwa kupatiwa hatimiliki. Vilevile, mpango wa urasimishaji wa maeneo katika Jiji la Dar es Salaam uliandaliwa ambapo viwanja **1,057** vilipimwa. Katika mwaka wa

fedha 2010/11, Wizara, itakamilisha Programu ya Taifa ya Kuzuia Ujenzi Holela na Kurasimisha Makazi. Programu hii ni dira ya kuzuia ujenzi holela na kuboresha makazi holela nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na MKURABITA itaendelea na kazi ya kurasimisha milki katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**Mipango ya Uendelezaji Vituo vya huduma na Miji mipya**

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na halmashauri za Jiji la Dar es Salaam iliendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa watu na magari katikati ya Jiji kwa kuanzisha vituo vya huduma za jamii katika maeneo ya pembezoni (*satellite centres*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, jumla ya wakazi **259** walilipwa fidia katika eneo la Luguruni na kutengewa viwanja mbadala **1,110** huko Kwembe Kati watakapohamia**.** Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kuendeleza Kituo cha Huduma cha Luguruni kwa kushirikiana na Mwendelezaji Mkuu Mshiriki (*Co-master Developer*) na kuandaa mipango ya maeneo ya Vyuo Vikuu ambavyo vina uhitaji mkubwa wa ardhi kama Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*Institute of Finance Management*) huko Bunju, pamoja na Chuo cha Tiba ya Afya Muhimbili huko Mloganzila - Kwembe.

65. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10 mchakato wa kuanzisha mji mpya wa Kigamboni uliendelea ambapo Mpango Kabambe wa mji huo ulikamilika. Mpango huo unaohusisha eneo la hekta 6,400 umeainisha matumizi mbalimbali yakiwemo ardhi ya makazi, biashara, viwanda, utalii na burudani. Matumizi mengine ni shughuli za taasisi za serikali, miundombinu, michezo, maeneo ya wazi (*open spaces*) na huduma za jamii. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaratibu kuundwa kwa mamlaka maalum itakayosimamia utekelezaji wa ujenzi wa mji mpya.

**Uandaaji Mipango ya Uendelezaji Vijiji**

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kuratibu kazi za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini. Lengo ni kuziwezesha mamlaka (Halmashauri za Wilaya) kupanga, kuidhinisha, kutekeleza, kufuatilia na kuhuisha mipango ya kina ya makazi katika maeneo yao ya utawala. Kwa mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikamilisha mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya makazi vijijini. Vilevile, mipango ya kina ya makazi imeandaliwa katika maeneo ya kati ya vijiji 20 katika Wilaya za Namtumbo, Manyoni, Bariadi na Babati. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itatafsiri mwongozo wa kuandaa mipango ya kina ya

makazi vijijini kwa lugha nyepesi ya kiswahili na kuusambaza kwa wadau mbalimbali zikiwemo halmashauri za wilaya na vijiji. Aidha, Wizara itashirikiana na halmashauri za wilaya za Manyoni, Babati na Bariadi kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya makazi ya vijiji iliyoandaliwa.

**Usimamizi na Udhibiti wa Uendelezaji wa Miji**

67. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI huweka kanuni na miongozo inayosaidia katika usimamizi na udhibiti wa uendelezaji wa miji nchini. Katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilitayarisha kanuni za sheria ya usajili wa maafisa mipangomiji ya mwaka 2007 na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matakwa ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itakamilisha marekebisho ya Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 kwa lengo la kukasimu mamlaka ya kuidhinisha mipango ya uendelezaji miji kutoka kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji kwenda katika ofisi za ardhi za kanda. Aidha, Sheria ya Mipangomiji ya mwaka 2007 itatafsiriwa kwa lugha nyepesi ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

## MIPANGO YA MATUMIZI BORA YA ARDHI

68. **Mheshimiwa Spika,** mipango ya matumizi bora ya ardhi iliendelea kuandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi za wilaya na vijiji. Mipango hiyo inasaidia kwa kiwango kikubwa katika uendelezaji wa ardhi na rasilimali zake, kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi, huwezesha upatikanaji wa maeneo ya ardhi kwa ajili ya wawekezaji, uhifadhi wa mazingira na huongeza ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na jamii ya wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini. Katika mwaka 2009/10, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya

Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ilitoa elimu kwa umma juu ya Programu za Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi. Wadau muhimu walishirikishwa ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri Wilaya na Asasi za Kiraia.

**Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji**

69. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kushirikiana na halmashauri za wilaya, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Asasi zisizo za Kiserikali

na wadau mbalimbali kuwezesha uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi ya wilaya na vijiji. Katika kipindi hicho Tume ilikamilisha kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya wilaya nane za Longido, Bariadi, Mtwara, Pangani, Mkinga, Muheza Ngorongoro na Babati.

70. **Mheshimiwa Spika,** mwaka jana nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa wizara itatayarisha mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **100** nchini. katika kipindi hicho, tayari vijiji **128** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya za Kilosa, Mpanda, Nkasi, Kongwa, Kiteto, Kisarawe, Misenyi, Kigoma Vijijini, Kilosa, Uyui, Kilombero, Babati, Longido, Bariadi, Namtumbo, Ulanga, Singida, Bagamoyo, Monduli na Morogoro Vijijini. **(Angalia Jedwali Na. 9)**. Katika vijiji hivyo, maeneo ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yametengwa kwa kushirikisha wananchi.

71. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itatayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa njia shirikishi katika **vijiji 150** katika wilaya zilizopo katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Arusha, Morogoro, Bukoba, Mtwara, Lindi, Tanga, Manyara, Mara, Singida na Ruvuma. Pia,

mafunzo kuhusu sheria za ardhi na mbinu shirikishi za utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi yatatolewa kwa watendaji katika ngazi ya wilaya zitakazoandaliwa mipango. Vilevile, Wizara yangu itaanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kutekeleza programu 3 ambazo ni programu ya Kilimo, Maji na Mifugo kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo, Mifugo na Maji. Tume kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itasaidia kupatikana kwa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Tume itafanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya ardhi hasa katika maeneo yenye migogoro, uhamiaji mijini kutoka vijijini, ushirikishwaji wananchi katika kuendeleza ardhi mijini na viwango vya matumizi ya ardhi mijini na vijijini. **Napenda kutoa wito kwa Wizara na Halmashauri za Wilaya zote kutenga bajeti ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi.**

## MAENDELEO YA NYUMBA

72. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta ya nyumba katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya nyumba nchini kutachangia katika kuongezeka kwa nafasi za ajira, kuinua vipato vya watu, kuchangia afya

njema, kuboresha mazingira ya kuishi na hivyo wananchi kuweza kupata maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Pamoja na juhudi za Serikali za kuanzisha Idara ya Nyumba na kuanza kuweka mazingira stahiki ya uendelezaji nyumba hapa nchini, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ya kutokuwa na mfumo wa kiutawala katika mamlaka za serikali za mitaa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara katika mwaka 2010/11 itawasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuanzisha mfumo wa kiutawala kwa mfano Idara au Kitengo kitakachoshughulikia masuala ya uendelezaji wa nyumba katika kila Halmashauri ya wilaya na majiji.

73. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mikopo ya Nyumba ya mwaka 2008 [*Mortgage Financing (special provisions) Act No. 17*] iliyoanza kutumika Mei, 2009 tayari benki tano (5) zimeanza kutoa mikopo ya kujenga na kununua nyumba. Benki hizo ni *Azania Bank Limited, Commercial Bank of Africa Ltd, International Commercial Bank, Stanbic Bank Limited* na *United Bank of Africa.* Ni matarajio kwamba benki zingine nazo zitaanza kutoa mikopo ya aina hiyo baada ya Serikali kuunda kampuni inayojulikana kama *Tanzania Mortgage Refinancing Company (*TMRC*).* Kampuni hii binafsi inamilikiwa na mabenki

ya hapa nchini itakuwa inatoa mikopo ya muda mrefu kwa mabenki, ili nayo mabenki yaweze kuwakopesha wateja wao mikopo ya nyumba ya muda mrefu (miaka 20 – 25 au zaidi) na yenye riba nafuu.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Nyumba na rasimu ya mwongozo wa kuanzisha na kuendeleza vyama vya ushirika wa nyumba hapa nchini. Kwa mwaka 2010/11, Sera ya nyumba itazinduliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali. Rasimu ya mwongozo wa kuanzisha na kuendeleza vyama vya ushirika wa nyumba itawasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao kabla ya kuanza kutumika, na utafiti wa hali ya nyumba nchini utafanyika.

75. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliendelea kuratibu Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali (*Revolving Housing Loan Fund*) unaotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ununuzi wa nyumba. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, mfuko ulitoa mikopo ya shilingi **2,363,502,144** kwa watumishi **218.** Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Mei, 2010 jumla ya shilingi **353,291,365.82** zilikusanywa kutoka kwa wanufaika wa mfuko huo. Kwa mwaka wa fedha 2010/11,

Wizara itaandaa utaratibu wa kuubadili mfuko huu uwe wa dhamana ili uweze kuwahudumia watumishi wengi zaidi.

**Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA):**

76. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(National Housing and Building Research Agency - NHBRA)* ni kufanya tafiti, kuelimisha, kukuza, kushauri, kuhamasisha na kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu. Lengo la Wakala ni kuinua na kuboresha viwango vya nyumba kwa kutumia vifaa vilivyotafitiwa na vinavyopatikana hapa hapa nchini, jambo ambalo litaongeza ubora wa maisha ya wananchi mijini na vijijini.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2009/10, maabara ya wakala imeboreshwa ili kuwezesha kupata matokeo bora ya utafiti. Uhamasishaji na mafunzo kwa vitendo yalifanyika katika wilaya za Dodoma mjini, Singida mjini, Manyoni, Morogoro mjini, Mvomero, Moshi vijijini, Bariadi, Kasulu, Tabora Vijijini, Ilala, Temeke na Kinondoni; na kutengeneza mashine za kufyatulia matofali yanayofungamana na kuzisambaza kwa wadau. Pia, uhamasishaji kwa wananchi

juu ya kuanzisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ulifanyika katika mikoa ya Tanga, Mara na Ruvuma. Ushauri wa kitaalam na ukandarasi juu ya utumiaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zilizotafitiwa ulifanyika katika wilaya za Mvomero, Ilala, Temeke, Korogwe na Same (**Angalia Jedwali Na. 10a &10b)**.

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2010/11, wizara itaendelea kufanya utafiti wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu zilizotafitiwa katika wilaya mbalimbali nchini; kujitangaza kupitia vyombo vya habari na kushiriki katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa kwa lengo la kusambaza teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba nchini; kushiriki katika uhamasishaji kwa njia ya semina na vitendo katika halmashauri za miji na wilaya zilizowasilisha maombi kwa wakala. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa huduma za ushauri kwa kutumia vifaa na teknolojia iliyofanyiwa utafiti na Wakala na kupatikana hapa hapa nchini. **Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuzihamasisha halmashauri za wilaya kutumia huduma za Wakala kwa kazi za ujenzi wa majengo mbalimbali hasa majengo ya umma**

**(madarasa, nyumba za walimu na zahanati) ili kunufaika na huduma za Wakala na pia kusambaza teknolojia.**

**Shirika la Nyumba la Taifa (NHC):**

79. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Shirika lilitumia Shilingi **bilioni 4.03** kugharamia miradi ya ujenzi wa nyumba **40** za makazi eneo la Medeli-Dodoma; jengo la ghorofa **5** la biashara eneo la Balewa – Shinyanga, majengo **6** ya biashara yenye thamani ya Shilingi **bilioni 14.7** yaliyojengwa kwa ubia kwa kushirikiana na sekta binafsi yalikamilika katika kipindi hiki. Shirika pia limekamilisha utekelezaji wa mradi wa ukandarasi wa ujenzi wa bweni la wasichana katika Chuo Kikuu cha Mzumbe wenye thamani ya Shilingi **milioni 976**, na nyumba za makazi Dar es Salaam (eneo la Regent Estate). Aidha, Shirika limetumia Shilingi **bilioni 5.3** kugharimia miradi iliyo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Miradi hii inahusu ujenzi wa nyumba **34** zinazoendelea kujengwa kwa ajili ya kuuzwa katika eneo la Mbweni JKT- Dar es Salaam; majengo **6** ya ghorofa yenye nyumba **48** za makazi eneo la Kibla Arusha; Awamu ya Pili ya ujenzi wa ghorofa mbili zenye nyumba 40 eneo la Medeli – Dodoma; na ujenzi wa nyumba **4** za makazi eneo la LDA – Arusha. Shirika pia linaendelea na ujenzi wa majengo **43** ya

biashara yenye thamani ya Shilingi **bilioni 96.6** yanayojengwa kwa ubia. Mingi ya miradi hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2010/

i. 11.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Shirika lilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **bilioni 35.9** kutokana na kodi za pango la nyumba linazozimiliki. Hadi kufikia Juni, 2010, Shirika lilikuwa limekusanya Shilingi **bilioni 33.6.** Makusanyo haya ni ongezeko la asilimia 24 yakilinganishwa na kiasi cha Shilingi **bilioni 27.05** kilichokusanywa mwaka jana kipindi kama hiki. Ongezeko hili linatokana na marekebisho ya viwango vya kodi kwenye nyumba za makazi yaliyoanza kutekelezwa Julai 2009 pamoja na uwezo zaidi wa kukusanya kodi na malimbikizo unaotokana na marekebisho ya Sheria Na. 2 ya 1990 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999.

81. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2010/11, Shirika linatarajia kukusanya Shilingi **bilioni 36** kutokana na kodi za pango. Shirika litatumia sehemu ya mapato hayo kulipia riba ya mikopo ya mabenki itakayochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, matengenezo ya nyumba, kuongeza hazina ya

viwanja na shughuli nyinginezo za maendeleo. Katika jitihada za kuongeza mapato na kumudu majukumu yake barabara, Shirika litaendelea kutumia fursa ya marekebisho ya sheria Na. 2 ya 1990 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 na Sheria Na. 11 ya 2005 kuwahamasisha wapangaji kulipa kodi kwa wakati. **Natoa wito kwa wapangaji kulipa kodi zao kwa wakati ili kuepuka kadhia ya kuondolewa kwenye nyumba na kunadi mali zao ili kufidia madeni.**

82. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2009/10 Shirika liliendelea kuyafanyia matengenezo majengo yake yapatayo **2,392**. Aidha, Shirika liliendelea kutenga asilimia 25 ya mapato yake yatokanayo na kodi za pango kila mwaka kwa ajili ya matengenezo. Matengenezo haya hufanywa kulingana na mpango maalumu unaolenga kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba zake zote katika kipindi cha miaka mitano (5) yaani, 2006/07 mpaka 2010/11. Katika kipindi husika, jumla ya majengo **867** na nyumba **2,543** zimefanyiwa matengenezo makubwa kwa gharama ya Shilingi **bilioni 7.4**. Kwa mwaka 2010/11 shirika litaendelea kutenga asilimia 25 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba linazozimiliki.

83. **Mheshimiwa Spika,** itatakumbwa kuwa mwaka 2008, Bunge lako tukufu lilipitisha sheria ya mikopo ya nyumba (*mortgage financing act*) na sheria ya umiliki wa sehemu ya jengo (*the unit titles act*). Sheria hizi zililenga kutoa fursa kwa waendelezaji wa nyumba kupata mikopo ya kujengea nyumba na pia kuzimilikisha kiurahisi kwa wanunuzi. Kwa kutumia fursa hiyo Shirika limeelekezwa kujikita zaidi katika kufanya biashara ya kujenga nyumba na kuziuza (*real estate developer*) kupitia mikopo ya benki badala ya kuwa mpangishaji na mkusanyaji wa kodi za pango tu (*Landlord*). Katika kutumia fursa hii, kwa mwaka wa fedha 2010/11, Shirika limejipanga kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa na utoaji wa ajira kupitia sekta ya ujenzi wa nyumba.

84. **Mheshimiwa Spika,** kulingana na mpango mkakati wa shirika wa miaka mitano ( 2010/11 – 2014/15), Shirika litaanza na ujenzi wa nyumba 1,000 katika mwaka 2010/11 kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa nyumba na hasa katika jiji la Dar es Salaam. Aidha, litaanza ujenzi wa majengo ya vitega uchumi na nyumba za makazi katika mikoa mbalimbali nchini. Miradi hii ni pamoja na majengo ya biashara katika maeneo ya Upanga, Magomeni na Lumumba (Dar es Salaam); Majengo ya biashara na makazi maeneo ya Sumbawanga – (Rukwa); Babati –

(Manyara); Mvomero – (Morogoro); Karume/Azimio – (Lindi), Barabara ya Boma – (Moshi), Shangani- (Mtwara), Kingo – (Morogoro) na Barabara ya Nyerere – (Mwanza); Medeli (Dodoma), na pia mikoa ya Shinyanga, Singida na Tabora. Aidha, Shirika linatarajia kujikita kwenye ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini kwa kushirikiana na wadau wengine. Miradi hii yote inakadiriwa kugharimu kiasi cha Shilingi **bilioni 100.** Katika utekelezaji wa miradi hii, Shirika linatarajia kukopa kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya fedha. Kwa mujibu wa mpango huu wa miaka mitano (kuanzia mwaka wa fedha 2011/12) Shirika litakuwa linajenga wastani wa nyumba 3,000 kila mwaka na mikoa yote itahusishwa katika ujenzi huu.

85. **Mheshimiwa Spika,** zoezi la kuhakiki wapangaji wa shirika lilianza kutekelezwa nchi nzima kuanzia mwezi machi, 2010. Lengo ni kubaini wapangaji haramu na wale wanaotumia nyumba za Shirika kwa manufaa binafsi. Katika kipindi hiki kifupi jumla ya wapangaji **379** wamebainika kupangisha nyumba kwa watu wengine pasipo idhini ya Shirika. Aidha, wapangaji 28 wamepangisha nyumba kwa watu wengine baada ya kupewa vibali na Shirika. Kwa mwaka wa fedha, 2010/11 shirika litaendelea na mchakato wa kufuta upangaji wa

wapangishaji na kuhalalisha upangaji kwa watumiaji wa sasa. Aidha, hatua kali za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi ya watumishi wa Shirika watakaobainika kushiriki katika njama hizi za kujinufaisha binafsi kupitia upangishaji haramu.

86. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita, niliarifu kuhusu azma ya NHC kuuza baadhi ya nyumba zake ambazo gharama za kuziendesha ni kubwa kuliko mapato. Zoezi hili linahitaji maandalizi makubwa, maandalizi hayo yanahusu kuwatambua wapangaji wa nyumba hizo na uwezo wao wa kulipia ununuzi, kutafuta benki zitakazowakopesha fedha za kununua hizo (*flats*) na pia kuwaelimisha wahusika taratibu za umilikishwaji nyumba hizo chini ya sheria ya umilikishaji wa sehemu ya jengo. Maandalizi haya yakikamilika ndipo zoezi la uuzwaji wa nyumba hizi utaanza kutekelezwa. **Napenda kurudia tena kwamba NHC watauza sehemu tu ya nyumba zao zinazowapa hasara kuziendesha na siyo nyumba zote.**

## HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU

87. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kutoa huduma za utawala na usimamizi wa rasilimali kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi.

Maeneo yaliyozingatiwa ni uimarishaji utawala bora, maadili mema ya utendaji kazi, kujali wateja, kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma kwa wakati. Vilevile, mapambano dhidi ya janga la UKIMWI yaliimarishwa kwa kuhamasisha watumishi kujikinga na kupima afya zao kwa hiari.

**Usimamizi wa Rasilimali Watu**

88. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara yangu iliajiri watumishi wapya **89,** kuwapandisha vyeo watumishi **135,** kuwathibitisha kazini watumishi **131** na kuwapatia mafunzo watumishi **115.** Lengo likiwa ni kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi za Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya **79** na kuwapatia mafunzo watumishi **120.**

89. **Mheshimiwa Spika,** baada ya wizara kubainisha mahitaji ya watumishi wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri, ilifanya mazungumzo na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), inayosimamia Halmashauri ili Halmashauri zione umuhimu wa kuajiri watumishi wanaohitajika na kuondoa upungufu mkubwa uliopo. Watumishi wapya watakaoajiriwa mwaka 2010/11 katika Halmashauri wataimarisha na kuleta ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi. Lengo ni kuajiri wataalamu wa Sekta ya

ardhi moja kwa moja kutoka vyuoni na kuwapangia vituo kwenye Halmashauri zenye upungufu wa wataalam hao.

**Mazingira Bora ya Kazi**

90. **Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha mazingira ya utoaji huduma, Wizara yangu ilikamilisha ukarabati wa jengo la Wizara ghorofa ya pili na sehemu ya maegesho ya magari ya viongozi. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itajenga kituo cha huduma kwa wateja (*Customer Service Centre*), pamoja na kukarabati sehemu ya mbele ya jengo (Ardhi House). Vilevile, Wizara itajenga jengo kwa ajili ya ofisi ya ardhi ya kanda ya Ziwa (Mwanza) na itaanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la Upimaji na Ramani (Ramani House).

**Usimamizi wa Raslimali**

91. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara iliendelea kusimamia rasilimali zake kwa kutumia mifumo ya elektroniki iliyojengwa ambayo ina ingiza na kutunza kumbukumbu mbalimbali zinazohusu rasilimali watu (*Human Resource Management*) magari (*Vehicles Management*), kompyuta, na kumbukumbu za wateja wanaofika wizarani kupata huduma (*Visitors Management*). Mifumo hii ya usimamizi

wa rasilimali inasaidia katika kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati ya matumizi ya rasilimali zilizopo.

**Mapambano Dhidi ya Janga la UKIMWI**

92. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kuwahudumia kiafya watumishi wake wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (VVU). Mkakati wa kuwaleta watoa ushauri nasaha na kupima UKIMWI kwa hiari ulitekelezwa ambapo watumishi wengi wamehamasika kutambua hali ya afya zao. Katika kipindi hicho, watumishi 350 walijitokeza kupatiwa ushauri nasaha na kupimwa afya. Huduma ya dawa na lishe iliendelea kutolewa kwa watumishi waliojitokeza kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI kila mwezi. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendeleza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuendelea kuwapatia huduma watumishi walioathirika.

**Elimu, Habari na Mawasiliano**

93. **Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa habari sahihi na kwa wakati kuhusu Wizara na Majukumu yake ni muhimu sana katika kudumisha Utawala Bora na Uwajibikaji. Katika mwaka 2009/10, Wizara iliendelea kuboresha mawasiliano kwa umma kwa njia ya redio na televisheni pamoja na kushiriki katika

maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Wiki ya Utumishi wa Umma na Nane Nane. Lengo ni kuendelea kuwaelimisha wananchi na Wadau juu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea kuboresha mawasiliano kwa kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali.

**Vyuo vya Ardhi**

94. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kuvisimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ambavyo vinatoa mafunzo ya Upimaji Ardhi na Urasimu Ramani katika ngazi ya Diploma, Umiliki Ardhi na Uthamini pamoja na Uchapaji Ramani katika ngazi ya cheti. Katika mwaka 2009/10, idadi ya wahitimu ilikuwa **109** kati yao **52** walitoka Chuo cha Ardhi Tabora na **57** walitoka Chuo cha Ardhi Morogoro. Kwa mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea na upanuzi wa Chuo cha Ardhi Tabora kwa kujenga mabweni, madarasa na maktaba ili kuongeza idadi ya wanafunzi katika Chuo hiki.

**CHANGAMOTO**

95. **Mheshimiwa Spika,** changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi ni pamoja na: -

- Ardhi iliyopimwa na kumilikishwa inakadiriwa kuwa ni asilimia moja tu, hali hiyo imesababisha ardhi kutotumika ipasavyo na kusababisha migogoro ya ardhi kwa watumiaji mbalimbali.
- Ufahamu mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa Hatimiliki, na leseni za makazi katika kuzitumia kama dhamana katika vyombo vya fedha ili kujiletea maendeleo.
- Wizara kutokuwa na mfumo thabiti wa utunzaji wa kumbukumbu za sekta ya ardhi;
- Sekta ya ardhi katika Halmashauri za miji na wilaya kuendelea kutotengewa fedha za kutekeleza majukumu yao;
- Upungufu mkubwa sana wa wataalam wa sekta ya ardhi katika halmashauri za miji na wilaya;
- Wilaya na vijiji kutokuwa na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi.
- Riba kubwa kwa wananchi wanaokopa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba inayotozwa na mabenki ambayo ni kati ya asilimia 17 na 25 kwa mwaka.
- Viwango vya fidia kwa ardhi na mazao vinalalamikiwa na wadau wengi.

- Upungufu mkubwa wa nyumba mijini na wingi wa nyumba duni vijijini.

**Utatuzi wa Matatizo /Changamoto Zilizojitokeza**

96. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea kukabiliana na changamoto zilizojitokeza kwa kuchukua hatua zifuatazo: -

- Kuendelea kuweka mfumo wa alama za upimaji wa ardhi (*Geodetic Reference Frame*) ambao utawezesha kuharakisha upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani kwa gharama nafuu;
- Kujenga kituo cha kupokelea picha za anga (*Direct Satellite Receiving Station*) nchini ili kurahisha upatikanaji wa picha za anga ambazo matumizi yake ni pamoja na kurahisisha upimaji wa ardhi;
- Kuongeza kasi ya kupima ardhi na mashamba kwa ajili wa wawekezaji (*land bank*), kupima mashamba ya wanavijiji na urasimishaji wa maeneo yaliyojengwa bila kupimwa; na kuanzisha ofisi za ardhi za kanda ili kusogeza huduma karibu na wananchi.
- Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi; na Benki Kuu ya Tanzania imewezesha kuundwa kwa kampuni inayojulikana kama *Tanzania,*

*Mortgage Refinancing Company* (TMRC). Kampuni hii binafsi inamilikiwa na mabenki ambayo yamenunua hisa kwenye kampuni hiyo na hivyo kuongezea mtaji wa kukopesha mabenki ili nayo yaweze kutoa mikopo ya nyumba kwa muda mrefu (miaka 20-25 au zaidi) na kwa riba nafuu;

- Kuyawezesha mabaraza ya ardhi na nyumba ya Wilaya kwa kuyapatia vitendea kazi, kufungua mabaraza mapya na kuongeza idadi ya vikao vya kusikiliza mashauri kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi.
- Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umilikishaji wa ardhi kisheria;
- Wizara kwa kushirikiana na HAZINA na TAMISEMI zitasimamia fedha zinazorejeshwa kwenye halmashauri (20% ya makusanyo yao) na kuhakikisha kwamba zinatumika kuendeleza sekta ya ardhi kama mwongozo wa fedha hizo unavyoelekeza; na pia kuangalia uwezekano wa kuongeza asilimia hiyo.
- Kutekeleza mradi wa *Land Information System* uliopendekezwa na Mtaalam Mwelekezi *(Swedesurvey/International Land Systems);*
- Kuzijengea uwezo halmashauri za miji na wilaya ziweze kuandaa mipango ya uendelezaji miji na kuitekeleza;

- Kuongeza kasi ya kusambaza matokeo ya tafiti na kutoa mafunzo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi.
- Rasimu ya sheria ya uthamini inaandaliwa na viwango vya fidia vinaendelea kuishwa ili viendane na bei ya soko.
- Kuanda Mpango/Programu maalumu ya uhamasishaji na uwezeshaji wa ujenzi wa nyumba bora vijijini ili kuondokana na nyumba duni za nyasi na udongo.

**SHUKRANI**

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya wizara yangu napenda kuwashukuru wadau wote walioshirikiana nasi mwaka 2009/10 katika kutekeleza majukumu yetu. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GTZ), Denmark, Uingereza, Sweden na Uholanzi kupitia Mradi wa "*Business Environment Strengthening for Tanzania*" (BEST) na Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) na UN – Habitat.

98. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kushukuru sekta binafsi kwa kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na wizara yangu katika kuboresha maisha ya watanzania.

Shukurani za pekee ni kwa Waheshimiwa Wabunge kwa michango na hoja zao mbalimbali zilizohusu wizara yangu. Naomba muendelee kuwa wadau muhimu wa sekta ya ardhi ndani na nje ya Bunge la Tanzania.

99. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, **Bw. Patrick Rutabanzibwa,** kwa ushirikiano mkubwa alionipa kwa kipindi kifupi tangu ahamishiwe katika wizara hii. Pia, ninawashukuru Wakuu wa Idara, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, watumishi na wataalamu wote wa wizara kwa kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu. Naomba waendelee na moyo wa kuchapa kazi hususan katika kipindi chote hasa katika kipindi hiki cha kurahisisha ufanyaji biashara nchini (*Doing Business*) kwa kuwa sekta ya ardhi ni mwezeshaji mkuu wa sekta zote.

**HITIMISHO**

100. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia mwelekeo wa Serikali wa kuelekeza nguvu zake katika kuimarisha kilimo, Wizara yangu ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa ardhi inapatikana kwa ajili ya mashamba makubwa na viwanda vya mazao yatokanayo na kilimo. Aidha, matumizi mengine makubwa ya ardhi

yakiwemo ya uendelezaji wa nyumba (*Real Estate Development*), mahoteli, viwanda n.k. yanatengewa ardhi ya kutosha. Haya yote yatatekelezwa iwapo HAZINA ya ardhi itaanzishwa na kuimarishwa. Vilevile, baada ya kukamilika kwa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine ina jukumu la kuhakikisha kuwa maeneo yenye migongano na migogoro sugu ya matumizi ya ardhi yanapatiwa ufumbuzi. Kufuatia hili, Wizara yangu itaendelea kuhakiki, kupanga matumizi ya ardhi, kupima, kusajili na kutoa hati katika maeneo hayo ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki na hivyo kuondoa migogoro kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. **Natoa rai kwa Mamlaka na Taasisi mbalimbali kutoa ushirikiano unaotakiwa kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kwa lengo la kuwaondolea wananchi umaskini.**

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2010/11

101. **Mheshimiwa Spika,** ili Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2009/10, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo:-

**(i) Mapato:**

- Mapato ya Serikali (sh.) **20,641,200,000**

**(ii) Matumizi ya Kawaida**

- Matumizi ya Mishahara (sh.) 6,423,295,000
- Matumizi Mengineyo (OC) (sh.) 25,159,688,000

**Jumla Shilingi** **31,582,983,000**

**(iii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

- Matumizi ya Maendeleo (sh.) **22,265,078,000**

Jumla ya Matumizi ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Maendeleo ni Shilingi **53,848,061,000**.

102. **Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena wewe, na pia waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.ardhi.go.tz.

103. **Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**